HOTUBA YA MKURUGENZI WA MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA DKT. AGNES KIJAZI KWENYE UFUNGUZI WA WARSHA YA WADAU KUPITIA NA KUTOA MAONI KATIKA RASIMU YA MPANGO WA KITAIFA WA UBORESHAJI WA HUDUMA ZA HALI YA HEWA TANZANIA; TAREHE 10/02/2017

Wakurugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa;

Wawakilishi kutoka Taasisi Washirika wa Utekelezaji wa Programu ya GFCS;

Wawakilishi kutoka Idara Mbalimbali na Mashirika ya Serikali na yasiyo ya Serikali,

Ndugu Wanahabari,

Mabibi na Mabwana,

Ni heshima kubwa kwangu kujumuika nanyi leo kwenye warsha hii muhimu yenye lengo la kupitia na kutoa mapendekezo ya kuboresha rasimu ya Mpango wa Kitaifa wa kuboresha na kuimarisha huduma za hali ya hewa hapa nchini "**National Framework For Climate Services (NFCS)**". Mkutano huu ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya kimataifa ya kuboresha na kuimarisha utoaji na utumiaji wa huduma za hali ya hewa (Global Framework for Climate Services (GFCS)) ambapo kwa Bara la Africa unaitwa "**Climate Services Adaptation Programme in Africa *on Building Resilience in Disaster Risk Management, Food Security,***

***Nutrition, and Health*"-** yaani programu ya kujenga uwezo barani Afrika kukabiliana na majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa, Usalama wa Chakula na Afya bora. Programu hii inafadhiliwa na Serikali ya Kifalme ya Norway.

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa niaba yangu binafsi napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa serikali ya Kifalme ya Norway kupitia Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) kwa kufadhili mradi huu. Pia napenda kuwashukuru washirika wote wanaohusika na utekelezaji wa mradi huu kwa jitihada za pamoja za kuhakikisha kuwa programu hii inatekelezwa kwa wakati na kutoa matokeo yaliyokusudiwa. Tunawashukuru sana Shirika la Hali ya Hewa Ulimwenguni kwa kazi kubwa ya kuimarisha hudama za hali ya hewa duniani na kwa jitihada zake za kusaidia nchi za Afrika katika kuboresha huduma hizo.

Ndugu Washiriki, Mabibi na Mabwana,

Utekelezaji wa programu ya GFCS ulianza kutekelezwa na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), mwaka 2012, ambapo nchi wanachama zilipewa mwongozo na kutakiwa kuanzisha mpango wa kitaifa wa kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa. Mpango huu unatoa fursa ya kuongeza nguvu, kuboresha na kuimarisha utoaji na utumiaji wa huduma za hali ya hewa na hivyo kusaidia kuhimili na kukabiliana na changamoto za ongezeko la matukio ya hali mbaya ya hewa zinazozidi kuongezeka kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa (Climate Change).

Kwa miaka michache iliyopita tumeshuhudia ongezeko la matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwa ni pamoja na ukame, Joto, upepo mkali na mvua kubwa zinazosababisha mafuriko na kuleta madhara makubwa kwa wananchi, miundo mbinu na shughuli zote za kiuchumi na kijamii. Hivi ni viashiri tosha vya namna hali ya hewa inavyobadilika na madhara yake kwa jamii duniani kote.

Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa matukio hayo yataendelea kuongezeka kwa idadi na ukubwa wa matukio hivyo ni jukumu letu wote kuweka mikakati ya kukabiliana na mabadiliko hayo ili kupunguza madhara kwa wananachi na mali zao.

Ndugu Washiriki, Mabibi na Mabwana,

Jitihada za pamoja za Serikali na mashirika yasiyo ya Kiserikali na Wadau wote kwa ujumla ni muhimu na zinahitajika kwa haraka ili kwa pamoja tuweze kuboresha na kuimarisha utoaji na utumiaji wa huduma za hali ya hewa na hivyo kuiwezesha Jamii na Nchi yetu kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa. Ni dhahiri kuwa hali ya hewa haina mipaka na inapotokea hali mbaya ya hewa huathiri sekta zote za kiuchumi na kijamii hivyo hatuna budi kuwa na juhudi za pamoja na kuweka mikakati ya kiutendaji, na mifumo ambayo itawezesha kwa pamoja kukabiliana na hatimaye kupunguza athari na maafa.

Mabibi na Mabwana,

Kama nilivyotangulia kusema kuwa lengo kuu la warsha hii ni kuwaleta kwa pamoja wadau wa hali ya hewa ili kupitia na kutoa

mapendekezo ya kuboresha rasimu ya Mpango wa kitaifa wa kuimarisha utoaji na utumiaji wa huduma za hali ya hewa. Mapendekezo yenu yatasaidia kuboresha Mpango huu pamoja na utekelezaji wake. Mpango huu utasaidia kuongeza wigo na ufanisi katika shughuli za Uangazi, na usambazaji wa taarifa za hali ya Hewa na hivyo kuchangia katika kuboresha kilimo, usalama wa chakula, afya na huduma nyingine zinazotegemea hali ya hewa.

Ndugu Washiriki,
Napenda kuhitimisha hotuba hii fupi kwa kuwakaribisha wadau wote na kuwashukuru tena kwa kutenga muda wenu na kushiriki katika warsha hii muhimu kwa maendeleo endelevu ya Nchi yetu. Michango yenu ni muhimu sana na tunaihitaji ili tuweze kuboresha rasimu hii ili kufaninkisha malengo ya warsha na malengo ya Mpango huu. Napenda pia kutoa shukrani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kitengo cha Maafa kwa Ushirikiano wao na Mamlaka ya Hali ya Hewa katika kuandaa rasimu hii.
Natangulia kuwashukuru sana kwa Michango yenu mtakayotoa na nawatakia Warsha yenye mafanikio.

Baada ya maneno haya machache napenda sasa kutamka kuwa warsha hii ya siku moja ya kupitia rasimu ya Mpango wa utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini imefunguliwa rasmi.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA